CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)
(Tanzania Teachers' Union – TTU)

P.O. Box 3077 DODOMA | Fax: 262323452
Cable: WALIMU DODOMA | Telephone: 262323451
E-mail: info@ttu.or.tz

Your Ref: ......................
Our Ref: AB.277/308/04/36

08 Februari, 2025

Makatibu wa Mikoa,
**CHAMA CHA WALIMU TANZANIA BARA.**

**YAH:- TANGAZO LA RATIBA YA UCHAGUZI MKUU WA CWT FEBRUARI – MEI 2025**

Somo hapo juu lahusika.

## 1.0 RATIBA YA UCHAGUZI

Ifuatayo ni ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa CWT kuanzia ngazi za matawi hadi Taifa.

### 1.1 Ngazi ya Tawi (Sehemu za Kazi)

Tarehe 10 Februari hadi 23 Februari, 2025 kuchukua na kurudisha fomu. Uchaguzi utafanyika kuanzia tarehe 24 Februari hadi 02 Machi, 2025. Chaguzi hizi zitafanyika katika Shule, Vyuo vya Ualimu (TTC), Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs), Wizara na Taasisi mbalimbali zenye wanachama pamoja na Taasisi zilizopo ngazi za Wilaya zinazojumuisha ofisi za Elimu za Wilaya na Maafisa Elimu ngazi za Kata.

### 1.2 Ngazi ya Wilaya

Tarehe 10 Februari, 2025 hadi 11 Machi, 2025 kuchukua na kurudisha fomu. Uchaguzi utafanyika kuanzia tarehe 17-28 Machi, 2025.

**Office Bearers**

| | |
|---|---|
| 6. President | Ms. Leah L. Ulaya |
| 7. Vice. President | Mr. Suleiman M. Ikomba |
| 8. General Secretary | ...................................... |
| 9. Ag. Gen. Secretary | Mr. Joseph M. Misalaba |
| 10. Acting National Treasurer | Mr. Nashon A. Kidudu |

*All correspondences to be addressed to the General Secretary.*

### 1.3 Ngazi ya Mkoa

Tarehe 17 Machi-15 Aprili, 2025 kuchukua na kurudisha fomu. Uchaguzi utafanyika kuanzia tarehe 20-30 Aprili, 2025.

### 1.4 Ngazi ya Taifa

Tarehe 01 Machi-29 Aprili, 2025 kuchukua na kurudisha fomu. Mkutano Mkuu wa Taifa utafanyika tarehe 28-29 Mei 2025, ambapo uchaguzi wa ngazi ya Taifa utafanyika tarehe 29 Mei, 2025. Wagombea wote watajulishwa mahali pa Mkutano kabla ya Mkutano Mkuu wa uchaguzi. Tarehe 01 Machi-29 Aprili, 2025 Vitengo vya Walimu Wanawake na Walimu wenye Ulemavu kuchukua fomu na vitafanya chaguzi zao tarehe 27 Mei 2025.

## 2.0 NAFASI ZINAZOGOMBEWA

### 2.1 Ngazi ya Tawi (Sehemu ya Kazi)

Mwakilishi wa sehemu ya kazi ambaye atakuwa ni Katibu wa Chama Sehemu ya Kazi (Tawi la Chama).

### 2.2 Ngazi ya Wilaya

Mwenyekiti wa Wilaya, Mwekahazina wa Wilaya, Mwakilishi wa Walimu Wanawake Wilaya, Mwakilishi wa Walimu Wenye Ulemavu Wilaya, Mwakilishi wa Walimu Vijana Wilaya (umri miaka 18-35) ambaye muda wake wa kuwa Mwakilishi unakoma anapofikisha umri wa miaka 35, Mwakilishi mmoja wa Shule za Awali, Wawakilishi wanne wa shule za Msingi, Wawakilishi wawili wa Shule za Sekondari, Mwakilishi mmoja wa Vyuo vya Ualimu, Mwakilishi mmoja wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs), Mwakilishi mmoja wa Uongozi na Taasisi nyingine za Elimu za Serikali zinazowajumuisha Maafisa Elimu Kata, Waratibu wa TRCs na Walimu Maafisa ngazi za Wilaya.

### 2.3 Ngazi ya Mkoa

Mwenyekiti wa Mkoa, Mweka Hazina wa Mkoa, Mwakilishi wa Walimu Wanawake ngazi ya Mkoa, Mwakilishi wa Walimu wenye Ulemavu ngazi ya Mkoa, Mwakilishi wa Walimu Vijana (umri miaka 18-35) ngazi ya Mkoa, Mwakilishi wa Wenyeviti

**Office Bearers**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | President | Ms. Leah L. Ulaya |
| 2. | Vice. President | Mr. Suleiman M. Ikomba |
| 3. | General Secretary | ...................................... |
| 4. | Ag. Gen. Secretary | Mr. Joseph M. Misalaba |
| 5. | Acting National Treasurer | Mr. Nashon A. Kidudu |

***All correspondences to be addressed to the General Secretary.***

wa Wilaya kwenye Baraza la Taifa, Mwakilishi wa Mkoa kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa na Wawakilishi wa CWT kwenye vikao vya TUCTA ambao watatokana na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CWT Ngazi ya Taifa. Kwa nafasi za uongozi za TUCTA, mgombea anapaswa kuwasiliana na Katibu wa Mkoa au Wilaya ili kufahamu nafasi zilizogawanywa kwenye Mkoa wake.

**2.4 Ngazi ya Taifa**

rais, Makamu wa rais, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mweka Hazina, Mwakilishi wa Walimu Wanawake, Mwakilishi wa Walimu wenye Ulemavu, Mwakilishi wa Walimu Vijana (umri 18-35) na Wadhamini 3.

**2.5 Kitengo cha Walimu Wanawake ngazi ya Wilaya**

Mwenyekiti wa Kamatii ya Walimu Wanawake wa Wilaya, Mweka Hazina wa Kamati ya Walimu Wanawake Wilaya na wajumbe wanne wa Kamati ya Walimu Wanawake ngazi ya Wilaya.

**2.6 Kitengo cha Walimu Wanawake ngazi ya Mkoa**

Mwenyekiti wa Kamati ya Walimu Wanawake, Mweka Hazina wa Kamati ya Walimu Wanawake na wajumbe watatu wa Kamati ya Walimu Wanawake.

**2.7 Kitengo cha Walimu Wanawake ngazi ya Taifa**

Mwenyekiti wa Kamati ya Walimu Wanawake, wajumbe saba miongoni mwa Wawakilishi wa Kamati za Walimu ngazi ya Mkoa na mjumbe mmoja atakayechaguliwa miongoni mwa Wenyeviti wa Kamati za Walimu Wanawake wa Mikoa.

**2.8 Kitengo cha Walimu wenye Ulemavu ngazi ya Mkoa**

Mwenyekiti wa Kamati ya Walimu wenye Ulemavu atakayetoka miongoni mwa Wawakilishi wa Walimu wenye Ulemavu ngazi ya Wilaya.

**2.9 Kitengo cha Walimu wenye Ulemavu ngazi ya Taifa**

Wajumbe saba watakaochaguliwa kutoka miongoni mwa Wawakilishi wa Walimu wenye Ulemavu ngazi ya Mkoa.

## 3.0 FOMU ZA WAGOMBEA NAFASI MBALIMBALI

3.1 Fomu za wagombea kwa ngazi zote zitarejeshwa ifikapo saa 10.00 Jioni kwa tarehe husika katika ngazi zote.

3.2 Fomu za kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ikiwa ni pamoja na nafasi za uongozi wa vitengo vya Walimu Wanawake na Walimu wenye Ulemavu zitapatikana kwa Wawakilishi wa Chama sehemu ya kazi, ofisi za CWT Wilaya, ofisi za CWT Mikoa, Makao Makauu na kwenye tovuti ya Chama (www.ttu.or.tz).

## 4.0 SIFA ZA WAGOMBEA

Wagombea wa nafasi zote ndani ya Chama wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

4.1 Awe mwanachama kamili wa CWT ambaye ametoa ada ya uanachama kwa kipindi cha mwaka mmoja mfululizo na kuendelea na siyo kwa mkupuo.

4.2 Mwadilifu

4.3 Raia wa Tanzania

## 5.0 NYARAKA ZA KUAMBATANISHA

Wagombea wote watatakiwa kurejesha fomu za mgombea zikiambatanishwa na nyaraka zifuatazo:-

5.1 Hati tatu za mshahara (Salary slip) zilizochangiwa mfululizo kabla ya tarehe ya uchaguzi

5.2 Kivuli cha kitambulisho cha uanachama

5.3 Kwa wanaogombea nafasi za vijana, waambatanishe na cheti cha kuzaliwa.

## 6.0 WITO KWA MAKATIBU WA WILAYA NA MIKOA

Wito unatolewa kwa Makatibu wa Wilaya na Mikoa kusoma Katiba, Kanuni na Miongozo ya Chama katika kusimamia vema zoezi la uchaguzi.


**Office Bearers**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | President | Ms. Leah L. Ulaya |
| 2. | Vice. President | Mr. Suleiman M. Ikomba |
| 3. | General Secretary | ...................................... |
| 4. | Ag. Gen. Secretary | Mr. Joseph M. Misalaba |
| 5. | Acting National Treasurer | Mr. Nashon A. Kidudu |

***All correspondences to be addressed to the General Secretary.***

## 7.0 MIIKO YA UCHAGUZI

Wagombea wanatakiwa kuzingatia Kanuni ya 6.0 ya Uchaguzi wa Chama cha Walimu Tanzania Toleo la 5 la mwaka 2025 ambayo imeainisha miiko ya uchaguzi, ambayo ni:-

(a) Ni mwiko kwa kiongozi yoyote kwa maneno au kwa vitendo kumpendelea au kumsaidia kupata ushindi mwombaji mmoja kuliko mwingine miongoni mwa wagombea.

(b) Ni mwiko kwa mwanachama na kwa mwombaji yoyote wa nafasi ya uongozi kwa maneno au kwa vitendo, kutumia ukabila, dini au fedha vitu (takrima) au vitendo vingine vyovyote vya rushwa kama njia ya kutafuta ushindi katika uchaguzi ikiwa ni pamoja na kutoa ahadi zisizoweza kutekelezeka.

(c) Ni Mwiko kwa kiongozi yoyote au mwombaji yoyote wa ngazi ya uongozi au mwanachama yoyote aliyekabidhiwa dhamana ya usimamizi/uangalizi wa uchaguzi kufanya vitendo vya ukiukaji kanuni na taratibu za uongozi.

(d) Ni mwiko kutumia karatasi za kampeni nje ya utaratibu wa CWT au kutumia vishawishi vya aina yoyote ile kwa minajiri ya kupata kura.

(e) Ni mwiko kwa mgombea yoyote kufanya kampeni zenye hila dhidi ya mgombea mwingine.

(f) Kampeni zenye nia ya kupakana matope na kudhalilishana zitahesabiwa kuwa ni ukiukwaji wa Kanuni za Uchaguzi.

(g) Kiongozi au mgombea yoyote atakayethibitika amevunja kifungu chochote cha kanuni hii atanyang'anywa ushindi alioupata na hataruhusiwa kugombea uongozi ndani ya CWT kwa kipindi cha miaka mitano.

Chama kinawatakia heri na mafanikio kwa watakaojitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya Chama.

Wenu kazini,

KATIBU MKUU
CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)
MAKAO MAKUU - DODOMA

Mwl. Joseph M. Misalaba
**KAIMU KATIBU MKUU- CWT**

**Nakala**

1. Katibu Mkuu,
   Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,
   Mji wa Serikali Mtumba,
   S.L.P 2890,
   **DODOMA.**

2. Mkurugenzi Mkuu,
   TAKUKURU.
   S.L.P 1291,
   **411101 DODOMA.**

3. Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri,
   S.L.P 2890,
   **DODOMA.**